# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru 5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 4, Aprili 2019


Mhariri

# Vijana wanapokutana na Kristo

Muda unaokumbukwa sana wa 2019 ulikuwa ni ule wa ziara ya Papa Francis huko Panama pamoja na vijana, ambao historia zao zinaonyesha nguvu mpya na inayopyaisha ya kukutana.

Mang'amuzi ya maisha kama yale ya Erika de Bucktron au Alfredo Martínez Andrión na Nirmeen Odeh na wengine wengi hutoa ushuhuda wa jinsi Yesu Kristo alivyo makini na historia ya kila mmoja wetu, kuangalia mwelekeo wetu, tamaa yetu, kusikiliza mioyo yetu, kutoa maji kwa roho zetu kavu. Yeye yuko tayari kutusimamisha kwenye pembe za njia, kututazama machoni ili kutuambia jinsi anavyotupenda. Vijana hawa walielezea jinsi umasikini wa kimwili na wa kiroho ulivyowafanya kuishi katika kutengwa na jamii, uliosababisha wateseka kwa upweke wa kutisha. Kwa kukutana tu na macho ya Kristo, ambaye aliwapokea kama Baba anavyofanya kwa watoto wake, waliweza kupanda mlima ili kujiachia kukumbatiwa na Upendo, ambao uliwabadilisha kuwa mashahidi wa ufufuko wa Yeye ambaye hutoa na ambaye haombi kurudishiwa kamwe.

Uwepo wake, ulioanza na ujio wa Yesu kati yetu, unaendelea kupyaisha siku na siku katika njia za dunia nzima kwa wote walio na kiu na njaa ya kukutana naye.

Mara nyingi tunashangaa, kama bado kuna nafasi ya roho wa Mungu kwa Binadamu katika dunia iliyoendelea sana katika teknolojia.

Bila shaka mtindo mpya wa kuhusiana na ulimwengu, kupitia vyombo vinavyowezesha umuungniko wa haraka, lakini daima wenye maadili na ambao huwavuta vijana wengi, kwa kweli yanabaki mang'amuzi ya upweke mkubwa. Na ni katika hali hii hasa ambapo roho husukuma kutamani mahusiano muhimu bila shaka, mikutano yenye uhai, yenye uwezo wa kurejesha binadamu kwenye utu. Kwa hiyo kiini cha maadili ambapo tunaweza kujenga upyaisho wa kweli, mkutano wa kweli unaoeleweka kama mabadiliko ya furaha ya uwepo wetu kutoka hatua moja hadi nyingine, ni yale ya kujifahamu kama binadamu mwenye mang'amuzi ya juu, ambayo ushahidi wake wa juu na usio na shaka ni Msalaba.

Leo zaidi ya jana, Kristo anaomba kutoka kwetu sisi tuliowekwa wakfu, tulioitwa kufanya maisha yetu kuwa ushuhuda wa upendo, tuwe wasindikizaji wa safari, wenye uwezo wa kusikiliza na wa kumsindikiza jirani yetu, hasa vijana, kuelekea njia mpya, njia ya Emmaus, ile aliyoipitia Yesu Mfufuka.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- Vijana wanapokutana na Kristo 1

*Nafsi kwa Uongozi Mkuu*
- Sikukuu ya kumbukumbu ya miaka 185° ya Shirika - Acuto 2

*Toka Ulimwengu ASC*
- Wabolivia washiriki Kongamano huko Lima 3
- Marafiki wa Guatemala 3
- Sadbhawna na mazungumzo ya Kidini 4
- Mabadiliko ya utaratibu kwenye nyumba ya "Damu Azizi" ya Latina 5
- MRADI Kuonyesha wazi hali halisi ya Gerezani 5
- Kuwa mwanamke…taabu gani! 6
- "Mtakatifu wa kawaida, Mwanamke wa ajabu" Maria De Mattias 7
- Siku ya Vijana Duniani huko Panama 8
- Mkutano wa 25a wa Region ya Waabuduo Damu ya Kristo, Region ya Zagabria 9

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Semina ya tasaufi/roho ya ASC/JPIC Morogoro, Tanzania 10

*Ndani ya Shirika*
- Takwimu 11
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 13
- Sikukuu za kuzaliwa: tunasherehekea maisha 13
- Nadhiri za Kwanza 13
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 13

# Maadhimisho ya miaka 185° ya Shirika huko Acuto

Tarehe 4 Machi Uongozi Mkuu: Sr. Dani Brought, Sr. Matija Pavić, Sr. Wieslawa Przbylyo pamoja na Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, walishiriki maadhimisho ya miaka 185° ya kuanzishwa Shirika, huko Akuto.

Muda muhimu kwa Familia ya ASC ambao, kama alivyoeleza Mkuu wa Shirika katika barua aliyoiandika kwa ajili ya tukio hili, *unatualika kuishi muda huu kama fursa nzuri sana ya kujisikia zaidi katika umoja, kama mwili mmoja na kuhuishwa na upendo uleule wa kimisionari. Ndoto ya Maria De Mattias inaendelea katika maisha na kazi ya kila mmoja wetu aliyeitwa kuwa Mwabuduo Damu Azizi ya Kristo.*



Huko Acuto saa 16.30, *katika Kanisa dogo la Masista*, kama kawaida huitwa kanisa lililokaribu na Nyumba mama ya Waabuduo, watu wa Mungu waliungana pamoja na masista kwa ajili ya kusali rozari ya Damu Azizi. Sala ambayo ilitolewa kwa vizazi na ambapo Maria mwenywe aliifundisha na kuisali mara nyingi pamoja na watu, akiwa amejaa ule moto wa Upendo ambao ulimsukuma kujitoa mzima kwa Mungu na kwa ajili ya mpendwa jirani. Kusali rozari kupitia tena mafumbo ya Damu ya Kristo iliyomwagika, wakati wa uhai wake, hufundisha kuheshimu na kuisifu Damu ya Kristo: kielelezo cha *kipimo na wajibu wa Upendo wa Mungu kwa binadamu.*

Adhimisho kuu la Misa, liliongozwa na Padre Francesco Bonanno CPPS, na ilichangamshwa na nyimbo zilizoimbwa na kwaya ya watoto wa shule ya msingi ya Acuto iliyoongozwa na mwanamziki Maurizio Sparagna, mzaliwa wa Acuto. Baada ya adhimisho ilifuata maandamano pamoja na nyakati fupi za mapumico kwa ajili ya tafakari na sala, kwenye makazi alikoishi Maria De Mattias na ya Waabuduo wa Kwanza: Nyumba ya Pilozzi, Nyumba ya Frasca na Stefani. Wakati wa hija hii, mwalimu Sparagna pamoja na Sr. Angela Di Spirito ASC walichangamsha matembezi kwa masimulizi ya hadithi za maisha ya Mt. Maria De Mattias ambazo zilikuwa zikisimuliwa na Baba kwa mwanaye pamoja na mziki "Kimbia, Kimbia, Maria" ambao unasimulia mahangaiko ya utume. Maandamano yalifika kwenye Kiwanja cha Collegio, kwa sasa ni kitu cha Kiroho Maria De Mattias, ambapo Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika alitoa tafakari kuhusu umisionari wa Mt. Maria De Mattias katika leo ya historia; na baadaye aliwashukuru masista na wote waliofanya maandalizi ya maandamano. Jambo la kushangaza na la kugusa lilikuwa ni matembezi ya Wapolandi kielelezo cha furaha ya pamoja na cha shukrani kwa Mtakatifu. Adhimisho lilimalizika kwa muda wa karamu.

Kwa njia hii Waabuduo walitaka kukumbuka kuwa maisha kwa Mwanzilishi yalikuwa ni safari endelevu, yenye taabu, lakini pendevu, inayosukumwa na utafiti wa furaha kuelekea kwa Mungu tu na kwenye hamu ya kupeleka roho Kwake.

Siku tatu za sala ya maandalizi, ambazo ziliitangulia sikukuu, ziliunganisha Shirika zima, pamoja na wafanyakazi wetu walei na wanachama ASC, katika kwaya moja yenye shukrani na sifa kwa Bwana kwa zawadi ya Mt. Maria De Mattias kwa Kanisa na zawadi ya karama ambayo, kama mbegu inayozaa, Bwana aliiweka ndani ya moyo wake.





***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Foundation Bolivia

## Wabolivia washiriki kwenye Kongamano huko Lima

Januari, 14 watu wa Bolivia walishiriki Kongamano, lililofadhiliwa na kituo cha kiroho cha Damu ya Kristo huko Lima Perù, walikuwepo watu 250 karibu wote walikuwa watu wa Perù.

Wajumbe wa Bolivia walijumuisha ASC watatu na walei 11 ambao wanashiriki roho/tasaufi yetu kama wanachama au kama wafanyakazi pamoja nasi katika huduma. Wengi wao walifunga safari ya masaa 26 kwa basi kutoka Desaguadero kwenye mpaka kati ya Bolivia na Perù, wengine walilazimika kusafiri siku nzima na zaidi, wengi kutoka Marumpampa, Santa Cruz na Tarija.



Kwa hamu kubwa, walisikiliza mafundisho yaliyotolewa na Padre Barry Fischer, CPPS, na Sr. Sonia Matos, ASC, Dr. Juan Bosco Monroy na Isabel Chavez kuhusu tasaufi/roho ya Damu ya Kristo.

Ripoti zilifuatiwa na vikao vya vikundi ambavyo vilitoa fursa ya kuimarisha na kuchambua yaliyomo, pamoja na fursa ya kufahamu wajumbe wengine wa familia kubwa ya Damu Azizi.



Kabla ya kuja kwenye kongamano, kila mbolivia alifanya kazi ya kushirikisha mang'amuzi na mambo ya siku tatu pamoja na kikundi ambacho walikiwakilisha, ili kwamba wengine pia waweze kunufaika kwa maisha yao.

Lilikuwa tukio la baraka kwa kweli, lenye utajiri zaidi wa ukarimu mkubwa wa watu wa Perù ambao walituonyesha uzuri wa utamaduni wao.

***Sr. Anita Fearday, ASC***

Mission Guatemala

## Marafiki wa Guatemala



Mwezi uliopita Sr. Barbara Hudock na mimi tulikutana na kikundi cha "Marafiki wa Guatemala" kwenye parokia zilizoko kwenye nchi za Fort Recovery, Ohio.

Kila mwaka kikundi hiki hukusanya hela kwa ajili ya miradi ya Waabuduo Wamisionari walioko Guatemala, na Mwezi Februari, waliandaa chakula chenye pilipili pamoja na vitafunwa vitamu vingi vilivyoletwa na washiriki mbalimbali.

Ilipendeza kuhesabu marafiki wengi mbalimbali na kushukuru kwa miaka 19 ya utoaji wa msaada. Mungu ni mwema.

***Sr. Kris Schrader, ASC***

**Eneo la Bara: Asia**
**Region India**

# Sadbhawna na mazungumzo ya kidini

India, nchi yenye dini mbalimbali, kwa dunia ni mfano wa umoja katika utofauti ambapo watu wa matabaka tofauti na dini tofauti wanaishi katika maelewano. Katiba ya India ni ya pekee kwa asili yake, kutungwa kwake na sifa zake. Kwa kweli, taifa la India linaeleza matokeo ya mageuzi ya itikadi na kanuni za kijamii, kisiasa, kidini na kiutamaduni ambayo yameongoza jamii ya wanadamu kwa karne kadhaa. Jamii nyingi, tamaduni, dini na itikadi mara nyingi huingiliana na kusababisha migogoro na mapigano, uvamizi na vita. Hata hivyo, kanuni ya msingi ya "kuishi na kuruhusu kuishi" inakuza uvumilivu na ushirikiano. Tunu kama vile uhuru, usawa na udugu, haki na amani zinaweza kuonekana kama ndoto. Katiba takatifu ambayo inaongoza taifa, tunda la maono ya nguvu ya mababa waanzilishi, ilitolewa kwa Taifa mnamo Januari 26, 1950.

Tunajivunia kuwa raia wa taifa ambalo Katiba takatifu inazungumza lugha ya uhuru, usawa, haki, amani, udugu na mapenzi mema. Haki za msingi ambazo zinaleta matunda tu, sifa, heshima, ushirikiano na mshikamano, tunu zote na muunganiko wa yote yaliyo chini ya taifa la India. Mvuto wa tabaka, daraja, dini, utamaduni, lugha, taaluma au mtindo wa maisha hufanywa sawa na maadili ya juu kama vile: kifungo cha udugu, umoja na muungano, tunu asili za kibinadamu, ambazo pia hutokana na kanuni msingi na za kudumu za asili na za kiroho. Muunganiko wa karne nyingi wa taifa letu, kama watu wamoja, wenye dini mbalimbali, tamaduni nyingi na lugha nyingi, jamii yetu inaunganishwa na tunu zingine muhimu za kiroho na misingi ya maadili.

Sikukuu mbalimbali, kama Holi, Diwali, Eid, Krismasi huadhimishwa kwa namna iliyo sawa. Hata hivyo, hata kama mara kwa mara uelewano wa jamii unaingiliwa kutokana na tofauti ya makundi ya dini, wananchi wanapewa uhuru wa kushiriki dini yoyote na hata kubadilishana. Kwa kweli nchi haina dini rasmi.

Neno Sadbhawna ambalo kwa lugha ya Kihindi linamaanisha "usawa", mapenzi mema, hamu ya kutakiana mema ni yale yaliyotoa tunu za Katiba. Katika muktadha wa Kihindi, haya yote yanaonyesha maelewano na amani kati ya watu wake.

Roho na ukweli wa Katiba ni alama ya kupambanua ya demokrasia yetu. Changamoto na vitisho dhidi ya tunu za katiba zinaweza kushindwa kabisa kutokana na kuwepo kwa kanuni za Sadbhawna. Kazi ya kila raia ni kulinda utakatifu wa Katiba kwa kuzingatia kikamilifu kanuni zake.

"Sadbhawna thamani ya Katiba ya India" ilikuwa hasa mada iliyochaguliwa kwa ajili ya Kongamano. Mada ilifundishwa na Dr BR Ambedkar "India kwa wote", ina mizizi yake katika maadili ya Katiba zetu. , wanafunzi na wafanyakazi wa shule na wa vyuo, pamoja na watu hadhi mbalimbali za kijamii walishiriki katika kongamano, kupitia uandishi wa makala na insha juu ya mada mbalimbali . Tunaamini kuwa ushiriki kweye kikundi hiki cha harakati hii, ambapo Sr. Moly Parayil anafanya kazi kama Katibu, utawawezesha kufahamu zaidi umuhimu wa kuishi kwa umoja, amani, udugu nk.

***Sr. Moly Parayil, ASC***





Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

# Mabadiliko ya utaratibu kwenye Nyumba ya "Damu Azizi" ya Latina



Sisi wastaafu wa Taasisi, kwa ushirikiano na kikundi cha Masista, tulipanga, mchana siku ya Jumatatu, 19 Februari 2019, ilikuwa ni sikukuu ya carnevale ambapo tulivaa maski ili kuifanya iwe siku ya furaha kwa masista wote, kwa namna ya pekee wale walio wazee zaidi. Tukiwa tumevaa maski, kwa namna tofautitofauti, tulifuatano kwa safu na kucheza kwa kufuata mziki na nyimbo. Muda wa kushangaza ulikuwa wa kutoa zawadi za mashindano ya maski. Wote walipata tuzo. Jioni ilimalizika kwa chakula cha sherehe ya carnevale ambapo walishiriki wageni waliokuja bila kutarajiwa, walishangazwa kwa mambo yaliyotendeka ambayo wao hawakuyazoea. Shukrani kubwa iwaendee wote pamoja na watu binafsi waliohudumu kwa kuwezesha kufanyika tukio hili lisiloweza kusahaulika.

***Patrizia Moretta***
***Graziella Campobasso***

Region Italia

# MRADI Kuonyesha wazi hali halisi ya gerezani

Hatua kutoka kwenye wazo hadi kwenye mradi ni fupi kuliko kulipima. Dale Carnegie alisema: "Sisi sote tunaweza kufanya mambo ambayo hata hatufikiri kuwa tunaweza kufanya. Lakini ikiwa hutathubutu kabisa, hutajua uwezo wako ». Kuthubutu haimaanishi kujitupa bali kuwa na ufahamu wa kutathmini kila wazo na kujua jinsi ya kupokea ishara za kwanza za mradi.

Mradi hauzaliwi mezani. Huzaliwa kutokana na hamu ya kutoa jibu kwa hitaji. Kuingia kwangu kwenye gereza la Rebibbia haikuwa rahisi. Niliingiza miguu mle kwa moyo unaotetemeka. Mara moja niliguswa na nyuso za huzuni, dhaifu, zilizofifia. Hali hii iliamsha maumivu makali moyoni. Kosa kubwa lilikuwa ni kumwona kijana mwenye uso dhaifu, wenye huzuni asiyetaka chohote. Hapa kwa upande wangu iliibuka hali ya kusikiliza kwa makini, kwa ukimya, hali ya kuingia kwenye jeraha la kila mmoja, hali ya kuelewa maumivu, upweke, kuhisi mzingo wa miaka ya adhabu, huzuni ya kuwa mbali na familia zao. Hatua baada ya hatu, nilifikiri kuwa ulimwengu wote huu ungeweza kuingia kwenye kitabu. Lilizaliwa wazo la Shindano la Uandishi ambalo kwa sasa limefikia toleo la kitabu cha tano. Lakini ni kwa namna gani tunaweza kuufahamisha huu ulimwengu kwa wale wasioufahamu kabisa, unaoangaliwa kwa tuhuma, kama mahali pasipofaa, uliotengwa, unaohukumiwa?

Ndivyo lilivyozaliwa wazo la kuonyesha wazi mang'amuzi ya miaka niliyoishi sehemu ya wafungwa wengi wa jamii mbalimbali, wa tambaduni mbalimbali na kutoka sehemu mbalimbali, wakatoliki na wasio wakatoliki, kwa kuwafanya waingie majumbani na mioyoni, kuwafanya wapokee na washirikishe.

Hivyo sasa ASC, CPPS na walei wanajitolea kuufanya ulimwengu wa gerezani na shughuli zake zote ufahamike kati ya watu wa Mungu, kupitia parokia, vyama, shule, na mashirika mbalimbali. Gereza haliangalii tu watu wanaoishi ndani yake au wanaofanya kazi, bali huangalia yote kwa sababu huangalia udhaifu wa kiutu na madhara yake.

Kwa mang'amuzi ya kwanza, tutakutana Amelia, Umbria, kwenye Maktaba ya Mji L. Lama katika uwepo wa UNITRE (Università della terza età/ Chuo cha umri wa tatu) pamoja na dokta Edoardo D'Angelo na Prof, Maria Teresa Caccavale, Utawala na watu wa sehemu hiyo.

Yeyote mwenye nia ya kukaribia hali hii anaalikwa kujiunga na mradi huu, kwa sababu ushiriki wa wengi zaidi, huchukua maamuzi zaidi, ili kuweza kuwa ushuhuda wa Kanisa linalotoka, alipendalo Papa Francesco.

***Sr. Emma Zordan, ASC***

# HABARI MPYA KWENYE MAKTABA




## KUWA MWANAMPE... TAABU GANI!

*Kitabu Cha Anna Maria Vissani, Emilia Salvi, Patrizia Pasquini, kampuni ya utuoaji vitabu Velar*

Mjira ambapo Papa Francesco amekianzisha mtririko juu ya uthibitisho wa akili za kubuni za kike na madai mengi na tofauti ya wakati wetu, daima yanaendelea kuahidiwa.

Wakati huhuo, ili kusimamia urithi chanya katika mageuzi endelevu, ambapo majadiliano mengi, tafiti na machapisho, na hata matangazo ya sauti, kuna hitaji la haraka la kujua mchango pekee ambao mwanamke anaweza kuutoa kwa ulimwengu.

Licha ya hayo, uonevu dhidi ya wanawake unabaki na kuongezeka katika utamaduni wa Magharibi. kujiachia kwao au kinyume chake, uwepo wao wenyewe unatoa hofu: unaweza kuponya mahusiano msingi, ya mwanaume – mwanamke, yaliyorithiwa katika uumbaji na katika uwezekano wa kukua?

Pamoja na wanawake wengine, tuliamua kukutana kwenye Kituo chetu cha Kiroho, kila siku 15, kwenye meza ya chai kuongea juu yetu, kuzungumza mambo yanayotuhusu, kufanya utafiti pamoja juu ya maana ya kuishi hali yetu ya kuwa wanawake, na kuangalia wakati ujao kwa macho safi na wazi.

Kundi, lililoundwa na wanawake wenye umri kati ya 47 – 63, lilifurahia fursa nzuri ya kuongea mambo yao na kushirikishana mang'amuzi ya upevu, uhuru mkubwa wa mabinti waliokua sasa na, licha ya hisia kadhaa za kushindwa, kundi liliangalia kwa ari mpya nafsi zao.

Hamu ya kukusanya historia za maisha ili kuzitafiti katika mwanga wa mabadiliko ya miaka na hii kazi ya kumkomboa mwanamke ilikomaa katika mikutano hii, kati ya tabasamu na machozi. Ulimwengu wa wanawake leo haujafungwa ndani ya familia tu, bali pia unaonyeshwa katika ulimwengu wa nje, ule wa kazi na uhusiano na wengine. Lakini udhaifu wa muundo wa kibinadamu ambao kwa bahati mbaya unazidi kuonyesha mipasuko yake, majukumu yanawalemea wanawake wenye nyajibu ambazo haziwahusu.

Na labda "taabu" imewekwa kwa alama ya mshangao kwenye kichwa cha habari, kweli neno hili linataka kueleza mara nyingi ushindi, lakini mara nyingi pia udanganyifu, kujaribu kuzuia maumivu na uonevu katika mahusiano ya kiutu, kwa nguvu ya "kike".

Katika nyakati kama zetu ambapo ongezeko la mawasiliano yaliyochanganyikana na purukushani zake, kitabu hiki kinatuongoza kutafakari juu ya njia za maisha na mtazamo wa ndani wa utamaduni ambao unaonyesha jinsi wanawake, licha ya tofauti za kibinafsi za haki, bado wanaweza kuonyesha ulimwengu wenye mshikamano, katika uelewa kamili wa tunu zao.

Leo ni dhahiri kwa kila mmoja kwamba "jinsia ya kike" huzaliwa, lakini 'Mwanamke' ni kuwa, kwa kawaida... na ni katika maishi ya kutaka 'kupambana' kwa upande wa mtu binafsi ili kuonyesha kile ambacho kingebaki ndani daima na labda kuleta faida ya haraka zaidi au kidogo, inayoletwa na hali na mawazo yenye nguvu. Na hii ndiyo hasara ya "ule mpango mzuri wa vitu" anaoupenda sana Mtakatifu Maria De Mattias, ambavyo vinamzunguka kila mtu, hali, mazingira yetu, vikiomba kutengeneza mpango mpya, tajiri kwa kila misaada ambayo huruhusu mabadiliko yafanyike.

Kitabu kinamalizika kwa uamuzi thabiti: Leo, sio jana, wala kesho!

*Jumuiya ya Kituo cha Kiroho*
*"Juu ya Mlima"*

# "Mtakatifu wa kawaisda, Mwanamke wa ajabu" Maria De Mattias

Tarehe 4 Februari 2019 tulisherehekea miaka 214 ya kuzaliwa Mtalkatifu Maria De Mattias.

Sherehe ilitanguliwa na maandalizi ya kiroho katika kanisa la parokia yetu ya Mt. Andrzej Bobola huko Czestochowa. Wakati wa Triduo tulisali kwa ajili ya ASC, rozari ya Damu ya Kristo na kuimba nyimbo kwa heshima ya Maria De Mattias.

Jumapili (tarehe 3 Februari), katika mawasilisho mafupu kwenye vyombo vya habari, tulionyesha sura ya Maria De Mattias, Shirika letu, utume wake Poland na nje yake.

Misa ya sikukuu, ilianza saa 11:00, iliadhimishwa na paroko na Wamisionari wa Damu Azizi, walishiriki pia wanachama wetu, wanaparokia na marafiki zetu. Wakati wa Misa Takatifu kwaya ya parokia iliimba nyimbo kwa Mwanzilishi na kwa Damu ya Kristo. Mwishoni kulikuwa na baraka ya masalia ya Mtakatifu Maria De Mattias. Baada ya Misa vijana waliandaa onyesho fupi kwa mtindo wa mahojiano ya habari yaliyofanywa kwa ajili ya Mtakatifu Maria De Mattias kuhusu maisha yake na utakatifu. Vazi la wakati wa Maria De Mattias lilileta hamasa zaidi.

Kulikuwa na maonyesho ya picha ambazo zilionyesha mwanzo wa maisha ya Masista ASC huko Czestochowa – Kiedrzyn na historia ya nyumba pamoja na mabadiliko mbalimbali, shukrani kwa kazi ya Masista kwa miaka iliyopita, ilikuwa kweli mafanikio.

Baada ya maadhimisho kanisani, wote walipokea zawadi: biskuti za umbo la moyo pamoja na maneno yaliyoambatanishwa ya barua za Mt. Maria De Mattias.

Biskuti za umbo la moyo, jumla yake vipande 300, zilipikwa, kupakwa urembo mwekundu na Sista yuleyule, siku chache kabla ya sherehe.

Siku hiyo nyumba yetu ilifungua milango ili kupokea wageni wote waliokuwa wanakuja na wote walipata chochote kizuri juu ya meza kwa sababu wote walibeba kitu cha kushirikisha,

Sala na sherehe, kwa mara nyingine, zilitupa fursa ya kuelewa kwa kina karama ya "Mtakatifu wa Kawaida, Mwanamke wa ajabu" – Maria De Mattias.

***Justyna Machaj (aspiranti)***






# Siku ya Vijana Duniani huko Panama




Siku ya Vijana Duniani ilikuwa ni ndoto iliyosubiriwa sana na vijana wa Dokszyce ambayo hatimaye ilikuwa kweli. Ndani mwao iliamshwa hamu kubwa ya kwenda kwenye mkutano huu usio wa kawaida tangu 2016 mara baada ya kushiriki kwenye Siku ya Vijana Duniani huko Poland. Kupitia Mkutano huo, vijana walitaka tena mara nyingine kushirikisha imani yao na kujitajirisha kwa tunu za kikristo, kuonja roho ya umoja katika utofauti wa Kanisa na kuungana na mataifa mengine. Tulianza kutafuta msaada tukimtegemea Mungu na kusali: " Mungu iliwa ni mapenzi yako, utusaidie kupata vyanzo vya kifedha kwa ajili ya safari hiyo."

Ari ya vijana iliongezeka licha ya kuonekana ugumu na kutofanikiwa, tuliandika kwa mashirika mengi ili kutusaidia kufanikisha ndoto hii, ambayo imetimia, shukrani kwa ufadhili wa Mungu, kwa watu wenye mapenzi mema na kwa uvumilivu wa vijana. Tuliondoka tarehe 15 Januari ili kushiriki mikutano ya jimbo kwa ajili ya vijana huko Colonia na halafu huko Panama, mahali ambapo tulikutana na watu wenye mioyo wazi na wenye ukarimu mkubwa, walijishughulisha kwa ajili yetu ili tusikose kitu. Niliguswa kwa namna ya pekee na hali yao katika kupambana na maisha, kwamba hawakuwa wakitafuta usalama wa vitu na utajiri, bali walijua kufurahia chochote kile walichonacho. Sala yao ilikuwa nyofu, ya kawaida na isiyo na upendeleo, hawakuweka masharti, bali kwa unyenyekevu walikuwa na imani kwa Mungu.

Mwanamke mmoja alitushirikisha kuhusu kukosa uwezekano wa kwenda kwenye Siku ya Vijana Duniani, kwa hiyo alikuwa anafurahi kwa ajili ya uwepo wa vijana kwa kuwa ulimwezesha kuonja imani yao, matarajio mazuri na matumaini. Kukaa kwangu huko Panama pamoja na vijana kwa ajili ya kuwasindikiza ilikuwa ni zawadi kubwa ya Mungu, niliweza kushiriki shukrani kwa waandaaji na kwa watu mojamoja waliotusaidia kifedha na kwa masista wetu ambao walinipokea kazi huko Dokszyce. Huu mkutano pamoja na vijana wa dunia yote ulikuwa ni mang'amuzi ya kina ya umoja katika utofauti. Ushuhuda wa imani yao, unyofu wao na uaminifu uliimarisha imani yangu ili kuwa kila siku ushuhuda zaidi wa kuaminika wa Kristo. Zaidi ya Mkutano wa Siku ya Vijana Duniani maswali ya Papa Franceso yanasikika kwa nguvu ndani ya mioyo yetu: Unataka kuweka maisha yako katika mikono ya Kristo ili Yeye awe kiongozi wako? Unataka kumtetea mnyonge zaidi?, Je! Unataka kumezwa na roho ya kwenda na wakati, ya ufujaji wa mali au kuwa ushuhuda hai wa Kristo?...

Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya mang'amuzi mazuri sana, yenye utajiri na ya pekee ambayo tunaweza kushirikishana na wengine.



***Sr. Małgorzata Augustyn, ASC***

# Mkutano wa 25 wa Region ya Waabuduo Damu ya Kristo, Region ya Zagabria



Kuanzia tarehe 26-27 Januari 2019 Waabuduo Damu ya Kristo Region ya Zagabria walifanya mkutano wa Region wa 25 wenye mada "Njia za Huruma". Siku ya kwanza ya mkutano, pamoja na masista, walishiriki pia waamini walei, wanajumuiya wa jumuiya ya Damu ya Kristo na wanachama ASC.

Kwa washiriki wote haya yalikuwa mang'amuzi ya pekee, tunaweza kusema Pentekoste mpya. Masista 43 na walei 40 wanaotoka sehemu mbalimbali za Croazia na kutoka Bosnia – ed Erzegovina walitafakari na kushirikishana maisha na roho/tasaufi ya Damu ya Kristo, wakitathimini njia mpya za kutembea pamoja, wakitafuta kuwa na ndoto na kufanya mipango kwa ajili ya wakati ujao.

Sr. Ana Marija Antolović, Mkuu wa Region katika utangulizi na ufunguzi wa kazi ya pamoja, aliwasalimia washiriki wote na alisoma ujumbe ambao Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirka aliutuma kutoka Roma.

Sr. Daniela Anić alisoma ripoti, iliyoandalia kwa ajili ya kikao hiki yenye kichwa cha habari: Damu ya Kristo – chemchemi ya uhai na ya utakatifu", ambayo ilikuwa ni utangulizi mzuri kwa tafakari ya pamoja na mwaliko wa kuingia kwa kina kwenye utambulisho wa tafakari, wa pasaka na utume wa maisha katika Damu ya Kristo.

Katika mwendelezo wa kazi, masista wanne Waabuduo Damu ya Kristo na mlei mmoja mwanachama ASC, walitutajirisha kwa mashirikisho ya mang'amuzi yao ya miaka mingi ya kazi na ushirikiano katika uundaji wa makundi na uongozi wa jumuiya ya Damu ya Kristo. Katika kazi ya mashirikisho, kwenye makundi, tulitafuta kutathimini mambo tuliyofanya na kuainisha njia kwa ajili ya wakati ujao. Makundi tisa, manne yakiongozwa na Maisista na matano na walei, walileta majibu ya mashirikisho yao. Makundi yote katika mashirikisho wazi yenye utajiri sana, walitoa umakini kwa namna ya pekee kwa matumaini na mtazamo kwa wakati ujao, kutembea pamoja Maista ASC, Wanachama ASC na wanachama wa Jumuiya ya Damu ya Kristo (ZKK).

Tunda la kushirikishana pamoja na hitimisho yametupeleka kwenye maelezo ya mwisho ya Kauli mbiu ya mwisho ya Mkutano ambayo, baada ya hitimisho la kazi, ilitumwa kwa masista wote na walei wanashiriki tasaufi/roho yetu, kwa hamu kuwa katika wakati ujao safari yetu ya pamoja itakuwa bado yenye kuzaa matunda kwa ajili ya Kanisa na jamii.

***ASC wa Region ya Zagabria***







# Semina ya tasaufi/roho ya ASC/JPIC Morogoro, Tanzania

## Mada: kwa nini usiwe moto?

Katika tukio la Jubile ya Region yetu, miaka ya hamsini (50) ya baraka na neema tuliyopokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia karama ya Mwanzilishi wetu, Mt. Maria De Mattias, Uongozi wa Region ulitupa fursa ya kuimarisha maisha yetu ya kiroho kupitia semina ya kiroho iliyoandaliwa na CIS, yenye Mada "Kwa nini usiwe moto?"





Sr. Toni Longo na Sr. Rani Padayattil, wanatume ya CIS, wamekuja kutoka Roma kwa ajili ya kutusaidia katika kuitikia mwaliko wa Mungu, kufungua mioyo yetu kwa Roho Mtakatifu, Moto wa Upendo, ili kuweza kumfuata Yesu popote na hivyo tunamshukuru Mungu. Ulikuwa ni muda ambapo tulisali, tulisikiliza, tulifanya kazi na kushirikishana, muda kweli wa furaha na matumaini chini ya milima ya Uluguru. Ingawa kulikuwa na hali ya joto sana na unyevu, mioyo yetu ilikuwa wazi na tayari kupokea mwito wa Roho Mtakatifu ili kuweza kubadilishwa na kuwa MOTO kuelekea wakati ujao.

Ndiyoi! Tunataka na tunatamani kuwa MOTO.

Watekelezaji wa JPIC.



Wajumbe wa Yesu Kristo, tukishiriki utume wake (Luka 4: 16-21) katika sala na matendo.

### *JPIC KATIKA HUDUMA KWA AJILI YA AFYA*

Kadiri ya tasaufi yetu na utume wetu, mwito wa kuwatunza wagonjwa na waliotelekezwa tayari ulikuwepo mwaka 1969 wakati ASC wa kwanza walipofika kupanda mbegu ya upendo wa Mungu. Hivyo kwa kufuata mfano wao sisi ASC watanzania tunaendelea kushirikiana na Kanisa, pamoja na mashirika mengine na kujibu mwito wa Mtaguso Mkuu wa II wa Vatican, tunajishughulisha kutimiza kazi za huruma katika sala na matendo, kupitia msaada kwa yule mwenye hitaji kimwili, kihisia na kiroho:

- o Kwa kutoa elimu ya kuzuia magonjwa kwa wale walioambukizwa magonjwa sugu;
- o Kutoa mahitaji kwa walio maskini na waliotelekezwa;
- o Kusaidia familia za wale wanaosumbuliwa na matatizo ya akili, kuwashauri na kuwapeleka kwenye taasisi zinazoweza kuwasaidia;
- o Kusikiliza na kuzungumza na wale wanaohitaji faraja ya kiroho, ili waweze kupokea hali zao;
- o Kuwatunza akina mama na watoto.

### *KUJISHUGHULISHA NA UTUNZAJI WA VIUMBE*

Hivi ni baadhi ya vitu tunavyofanya ili kulinda uumbaji:

- • tunajitahidi kufanya usafi wa mazingira yetu ndani na nje;
- • tunatenga taka katika vyombo vitatu tofauti;
  - o Taka hatari
  - o Taka zisizo hatari
  - o Taka ngumu
- • Tumepanda miti kando ya hospitali yetu.
- • Tuna kitalu cha kuoteshea miti ambapo tunaotesha miti na maua kwa ajili ya kupanda kwenye bustani zingine.
- • Tunawapa elimu na ushauri wale tunaokutana nao, kuwashirikisha faida na hasara zinazotokana na mahusiano yetu na viumbe kwa kuviheshimu au kwa kutovijali.

Kila baada ya miezi mitatu au inapolazimu, tunakutana kushirikishana kazi zetu na kufanya tathimini, ili kuboresha huduma zetu, katika kuitikia wmito wa Yesu wa kutoa uhai kwa viumbe wote na kwa Karama ya Mt. Maria De Mattias.



***Sr. RoseHawa Hassan Tantau, ASC***

| TAKWIMU YA ASC KIMATAIFA ZILIVYOBORESHWA KUANZIA 31, DESEMBER 2018 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NCHI | Nadhiri za daima | Nadhiri za muda | wanovisi | wakandidati | Waliohamia shirika jingine | Exclaustrated | Walioacha | Marehemu | Jumuiya |
| | | | | | | | | | |
| Albania | 04 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 |
| Argentina | 07 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 03 |
| Australia | 11 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 |
| Austria | 2 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Belarus | 03 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Bolivia | 08 | 01 | 00 | 01 | 00 | 00 | 01 | 00 | 04 |
| Bosnia-Erz. | 41 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 09 |
| Brazil | 50 | 00 | 02 | 02 | 00 | 00 | 02 | 02 | 11 |
| Korea | 14 | 03 | 03 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 02 |
| Croatia | 111 | 00 | 02 | 00 | 00 | 00 | 01 | 01 | 19 |
| Philippines | 08 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 03 |
| Germany | 13+ | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 4+ |
| Guatemala | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 |
| Guinea B | 04 | 06 | 02 | 02 | 00 | 00 | 00 | 00 | 03 |
| India | 69 | 11 | 04 | 04 | 00 | 00 | 01 | 00 | 14 |
| Italia | 430 | 01 | 02 | 01 | 00 | 00 | 00 | 26 | 66+* |
| Liechtenstein | 15 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 | 01 |
| Msumbiji | 03 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Peru | 03 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Poland | 64 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 9 |
| Russia | 03 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Spain | 09 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 03 |
| Switzerland | 05 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Amerika | 175 | 02 | 02 | 00 | 00 | 00 | 00 | 06 | 21 |
| Tanzania | 66 | 15 | 04 | 00 | 00 | 00 | 01 | 00 | 09 |
| Vietnam | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 |
| Liberia | 02 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 00 | 01 |
| Jumla | **1.122** | **40** | **21** | **11** | **00** | **00** | **06** | **36** | **192** |

N.B. Unapokutana na alama ya+, inamaanisha tunataja jumla ya idadi za jumuiya au Sista wa Region nyingine.
* Ikihusishwa na makao makuu.

## Jumla

| | |
|---|---|
| Nadhiri za daima | **1.122** |
| Nadhiri za muda | **40** |
| Jumla ASC | **1.162** |
| Wanovisi | **21** |
| Wakandidati | **11** |
| Tot. ad altre congr. | **0** |
| Exclaustrated | **0** |
| Jumla ya walioondoka | **6** |
| Jumla ya waliofariki | **36** |
| Idadi ya jumuiya | **192** |

**Attachment 1**

| 2018- Ongezeko la masista na upungufu: Nadhiri za kwanza na Nadhiri za daima – Walioacha au kufariki | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nadhiri 1 | Walioondoka wa N. Muda | Wenye Nadhiri za daima | Walioondoka wakiwa N.daima | Kuhamia shirika lingine. | Deceased sisters |
| Albania | | | | | | |
| Argentina | | | | 0 | | |
| Australia | | | | | | |
| Austria | | | | | | |
| Belarus | | | | | | |
| Bolivia | | 00 | 00 | 01 | 00 | 00 |
| Bosnia-Erz. | | | | | | |
| Brazil | | | 01 | 02 | | 02 |
| Korea | | | | | | |
| Croatia | | | 01 | 01 | 00 | 01 |
| Philippines | | | | | | |
| Germany | | | | | | 00 |
| Guatemala | | | | | | |
| Guinea B. | 03 | 0 | | | | 0 |
| India | | 00 | 04 | 01 | 0 | 0 |
| Italy | | | 0 | | 00 | 26 |
| Liechtenstein | | | | | | 01 |
| Mozambique | | | | | | |
| Peru | | | | | | |
| Poland | 00 | 00 | 01 | 00 | 00 | 0 |
| Russia | | | | | | |
| Spain | | | | | | 0 |
| Switzerland | | | | | | |
| United States | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 | 06 |
| Tanzania | 00 | 01 | 00 | 00 | 00 | 00 |
| Vietnam | | | | | | |
| Liberia | | | | | | |
| Jumla | 04 | 01 | 07 | 05 | 00 | 36 |

**Attachment 3**




## Kalenda ya Uongozi Mkuu

**11 Aprili :** Hitimisho la ziara ya kichungaji kwenye Region ya Zagabria
**13 - 14 aprili:** Kurudi Roma kutoka Zagabria
**28 - 30 aprili:** Muda wa malezi na mwezeshaji Sr. Marian Murcia.

## Sherehe za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha ya



| | | |
|---|---|---|
| miaka 50 | | |
| **Sr. Maria Chiara Maselli** | 16/04/1969 | Italia |
| **Sr. Inês Paulo Albino** | 25/04/1969 | Guinea Bissau |
| miaka 70 | | |
| **Sr. Zvonimira Borščak** | 21/04/1949 | Zagreb |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Ida Marino** | 27/04/1939 | Italia |
| miaka 90 | | |
| **Sr. Blandina Hug** | 04/04/1929 | Schaan |
| **Sr. Antonietta Morello** | 15/04/1929 | Italia |



## Nadhiri za kwanza za:

**28 Aprili 2019 - Korea**

**Sr. Thi Ha Tran**



## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

15/03/2019 **Sr. Malvina Piccioni** Italia

**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*

...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
*Waabuduo Damu ya Kristo*
*Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu*
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 4, Aprili 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić** - Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams** - Kiingereza*
***Sr. Martina Marco** - Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz** - Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque** - Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz** - Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin** - Kijerumani*